# MANISPAA YA MOROGORO YANYAKUA TUZO 3 MAONESHO YA NANENANE 2020.



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, akiwa na timu ya Watumishi Manispaa ya Morogoro mara baada ya Manispaa hiyo kuibuka kinara wa maonesho hayo ya Nanenane ya mwaka 2020 katika Viwanja vya Kambarage Nyerere vilivyopo Manispaa ya Morogoro.*

Manispaa ya Morogoro imenyakua tuzo 3 katika Maonesho ya Nanenane yaliyomalizika Agosti 8,2020 yaliyohitimishwa na mgeni rasmi Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu katika Viwanja vya Kambarage Nyerere Mkoani Morogoro.

Tuzo ambazo Manispaa Morogoro imenyakua ni pamoja na Tuzo ya Halmashauri ndani ya Mkoa wa Morogoro, tuzo ya Manispaa na Majiji pamoja na tuzo ya jumla ya Kanda ya Mashariki.

Akizungumza Mara baada ya utoaji wa Tuzo, Mhe. Martine Shigela , Mkuu wa Mkoa wa Tanga, amesema tuzo za Manispaa Morogoro zimatokana na jitihada za Viongozi wao ikiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa Morogoro, pamoja na Ushirikiano mkubwa wa Watumishi wake kujitolea kwa hali na Mali katika kuleta uhamasishaji ikiwamo Maafisa Kilimo na Mifugo."

Nawapongeza Sana Manispaa Morogoro, hii mmestahili ushindi, mmejitoa Sana hongereni" Amesema Mhe. Shigela.

# JAFO AFURAHISHWA NA UJENZI WA SOKO KUU LA KISASA MOROGORO

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Selemani Jafo ameonyesha kufurahishwa na ujenzi wa soko kuu la kisasa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika ujenzi ambao umekamilika kwa asilimia 99 ambao umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 17.6

Akizungumza mara baada ya kutembelea na kuona maeneo

INAENDELEA UK... 05

# RC SANARE AONGOZA MAMIA YA WATU KATIKA KUMBUKUMBU YA WAHANGA AJALI YA MOTO MSAMVU.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare pamoja na viongozi wengine wameongoza mamia ya watanzania walioji-tokeza kwenye Makaburi ya kola kata ya Kichangani katika siku ya kumbukizi ya wahanga wa ajili ya moto iliyotokea Agosti 10,2019 eneo la Msamvu Manispaa ya Moro-goro.

Akizungumza na Waandishi wa habari, amewataka Wananchi kila mmoja kuwa na wajibu wa kuhakikisha anaendelea kuchukua tahadhari kwa kila kiashiria cha hatari kinachowe-za kupoteza maisha ya watu.

RC Sanare, ameviagiza Vyombo vya Ulinzi na Usala-ma, vyombo vinavyohusika na uokoaji kuendelea kusimamia taratibu na kutekeleza majuku-mu yao ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za haraka pale linapotokea tatizo lolote linalofanana na janga kama lililowakumba wananchi walio-poteza maisha yao eneo la Msamvu.



Mkurugenzi Manispa aya Morogoro, Sheilla Lukuba, akiongoza msafara katika ukaguzi wa Ujenzi wa Makaburi ya Wahanga wa ajali ya Moto Msamvu katika Makaburi ya Kola Manispaa ya Morgoro.

Aidha, aliendelea kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi , Taasisi na Mashiri-ka juu za hatua madhubuti za kukabiliana na majanga kama hayo pindi yanapotokea .

Alisema , Serikali iliweza kuratibu na kusimamia matiba-bu ya waathirika wote waliopatwa na tatizo hilo ikiwa ni pamoja huduma za kimatiba-bu kwa wale waliotibiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Moro-goro na wale waliopewa rufaa ya kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Wakati Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majali-wa, tarehe 10,03,2020 alivyo-tembelea makaburi haya , alitoa maelekezo ya kuhakiki-sha kila tarehe 10 mwezi Agosti ya kila mwaka iwe inafanyika kumbukumbu ya kuwakumbuka marehemu , alituelekeza kuhakikisha

INAENDELEA UK... 07


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti ... Sheilla E. Lukuba**
*Mkurugenzi Manispaa Morogoro*

**Mhariri Mkuu ... Lilian K. Henerico**
*Afisa Habari Manispaa*

Washiriki wasaidizi

**Issa B. Issa:** *Afisa Habari Msaidizi*

**Yusuph A. Mwamba**
*Afisa Habari Msaidizi*



*mawasiliano:* *simu: 023 - 2935242*
*E-mail: info@morogoromc.go.tz*
*S.L.P 166*

*Mitandao ya Kijamii*

*Website:* *www.morogoromc.go.tz*
*youtube:* *Morogoro Manispaa TV*
*instagram:* *Manispaa ya Morogoro*
*facebook:* *Manispaa ya Morogoro*

# MANISPAA YA MOROGORO YATOA JUMLA YA MILIONI 517,800,000/= MIKOPO KWA VIKUNDI.

Jumla ya shilingi milioni 517,800,000/=zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya uwezeshaji kwa vikundi 72, ikihusisha vikundi 44 vya wanawake na vikundi 22 vya vijana pamoja na vikundi 6 vya watu wenye ulemavu.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Sheria inayozitaka Halmashauri kutenga asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili mikopo ya uwezeshaji wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Akikabidhi hundi za mikopo Juni 17, 2020 katika viwanja vya Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege , Mkuu wa Wilaya ya Morogoro , Mhe. Regina Chonjo,amesema fedha walizokopeshwa zinapaswa kutumika kama chachu ya kuwaletea maendeleo.

"Nawapongeza wana vikundi wote kwa kukidhi vigezo vya kupewa mikopo na Manispaa ya Morogoro, leo nimewakabidhi hundi hii ya mfano mbele ya waandishi wa habari, ni imani yangu kuwa mtazitumia fedha hizi kwa malengo mliyojiwekea , hakikisheni mkopo huu unawanufaisha watu wote bila ubaguzi , naamini hakuna hata kikundi kimoja kitakachoniangusha , pia viongozi mliohudhuria hafla hii mtambue kuwa




*Hundi ya Mfano ya vikundi vya mikopo ya uwezeshaji kiuchumi Vijana, Wakina Mama na watu wenye ulemavu iliyotolewa na Manispaa ya Morogoro Juni 17,2020 kwenye maeneo ya Viwanja vya Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege.*

mmeingia mkataba wa kupewa mkopo kwa niaba ya vikundi vyenu , hivyo mfanye shughuli ya pamoja kama mlivyoandika kwenye maandiko yenu ya mradi, lakini hatutaishia hapa bali tutafanya ufuatiliaji wa kukagua utekelezaji wa miradi yenu kuona maendeleo yenu" Alisema DC Chonjo.

Aidha alisema Serikali ya

INAENDELEA UK... 09

# DAS WILAYA YA MOROGORO ATOA WITO KWA TAASISI MBALIMBALI KUJITOLEA KUSAIDIA WATU WENYE UHITAJI MAALUMU.




*) Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John, akiwa pamoja na timu ya maafisa Ustawi wa Jamii pamoja na Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro wakiwa katika picha ya pamoja na Watoto wanaoishi Makao ya kulelea Watoto yatima ya Mission To The Homeless.*

Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John, ametoa wito kwa taasisi mbalimbali, mashirika, wafanyabiashara na watu wenye mapenzi mema kujitolea kusaidia watu wenye uhitaji maalumu kwani kwa kufanya hivyo ni kutimiza amri kuu ya upendo ya Mwenyezi Mungu isemayo pendaneni kama mimi nilivyowapenda ninyi.

Ruth aliyasema hayo wakati akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe.

INAENDELEA UK... 06

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI






*Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Mstaafu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo, akikagua gari la kubebea wagonjwa lilokabidhiwa na Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood kwa Wananchi wa Manispaa ya Morogoro ( kulia) ni Katibu wa Mbunge, Ndg. Mourice Masala akimuonesha gari hilo wakati wa ukaguzi.*





*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa , (katikati) ,akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Choo cha mfano cha Mtoto wa Kike kilichopo Kata ya Boma Shule ya Sekondari Tubuyu Manispaa ya Morogoro. (kusho-to) Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro Bi Enedy Mwanakatwe (kulia) Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba.*



*Mkurugenzi wa Ukaguzi wa ndani TASAF Makao Makuu, CPA-Chris-topher Sanga,akikagua zoezi la uhakiki wa Wanufaika wa Mpango wa TASAF Kipindi cha pili Awamu ya Tatu kwenye Kata ya Cham-wino.*



*Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, akipata maelezo juu ya Teknolojia mpya ya kilimo cha kisasa bila kutumia udongo (Hydroponic ) katika Vipando vya Shamba darasa la Manispaa ya Morogoro katika Maonesho ya Nanenane mwaka 2020 Kanda ya Mashariki.*

# JAFO AFURAHISHWA NA UJENZI WA SOKO KUU LA KISASA MOROGORO

INATOKA UK... 01



*Waziri wa OR-TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo(katikati), kushoto Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Sanare na Kulia Katibu tawala Mkoa wa Morogoro Eng. Emannuel Kolobero wakiwa katika picha ya pamoja katika ghafla fupi ya ukaguzi wa soko kuu la kisasa Manispaa ya Morogoro*

mbalimbali katika soko hilo Mhe. Jafo amesema kuwa licha ya kuwepo na ujenzi wa miradi ya masoko katika Mikoa ya Mtwara, Dodoma, Njombe na Dar es Salaam ujenzi wa soko la Kisasa Manispaa ya Morogoro ni wa kipekee na wenye viwango vya hali ya juu kutokana na ujenzi huo kuwa umezingatia mahitaji ya wafanyabiashara kuwa wanataka nini katika soko hilo.

“Mimi huwa nakuja kukagua kazi sio kutembelea na nimefika mara nyingi katika soko hili,awali nilikuwa siridhishwi na kasi ya ujenzi ila leo binafsi nimefurahishwa sana baada ya kufika hapa na kuona jinsi wakandarasi wetu wazawa walivyoweza kujenga kwa ubora unaoridhisha. Hiki ni kitega uchumi kikubwa sana kwa Halmashauri na kitabadili mandhari ya Manispaa hii,kwa aliyefika hapa miaka mitano iliyopita leo hii akija anaweza kupotea hii ni heshima kubwa sana aliyotupatia Mhe.Rais Dkt John P.Magufuli kwa kuamua kutupa fedha za mradi mkubwa kama huu.”Alisema Jafo.

"Nampongeza sana Mhandisi aliyesimamia ujenzi huu,pia nawapongeza viongozi na watumishi wote wa Manispaa ya Morogoro kwa ushirikiano mliouonyesha katika utekelezaji wa mradi huu ,hii inaonyesha jinsi gani mlivyo makini katika usimamizi wa miradi,Manispaa ya leo siyo ya jana angalia sasa mna stendi ya Msamvu,mmejenga stendi ya daladala,haya ni mafanikio makubwa sana katika Serikali ya awamu ya tano"Aliongeza Mhe.Jafo.

Aidha Mhe. Jafo ameahidi kushughulikia changamoto ya msamaha wa ongezeko la thamani VAT na kuhahidi kuifikisha katika mamlaka husika kwa kuwa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia haitakiwi kutozwa kodi.

“Lengo la miradi hii ni kwa ajili ya kukuza Miji na kuzijengea Halmashauri uwezo wa kujitegemea swala la msamaha wa VAT ni changamoto inayoikabili miradi mingi inayosimamiwa na TAMISEMI na hapa naona tena changamoto hii inajirudia licha ya Mhe. Rais kutoa maelekezo kuhusiana na suala hili. Naomba nichukue changamoto hii na nitaiwasilisha kwa Waziri wa Fedha kwa utekelezaji."Alieleza Mhe.Jafo.

Mradi wa soko kuu unatarajiwa kuingizia Halmashauri mapato ya zaidi ya shilingi Bilioni 2.3 kwa mwaka na hii itapunguza kutegemea ruzuku kutoka Serikali kuu.



*Muonekano wa mbele wa soko kuu la kisasa Morogoro lilogharimu Tsh. bilion17 hadi kukamilika kwake*

# DAS WILAYA YA MOROGORO ATOA WITO KWA TAASISI MBALIMBALI KUJITOLEA KUSAIDIA WATU WENYE UHITAJI MAALUMU.

INATOKA UK... 09

Regina Chonjo wakati akitoa misaada mbalimbali kwa makao ya kulelea watoto wenye mahitaji maalumu Mgolole pamoja na Mission To The Homeless katika hafla fupi ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika iliyofanyika Juni 16,2020.

DAS Ruth , alikabidhi misaada hiyo kwa wawakilishi wachache wa watoto hao walioongozana na baadhi ya walezi wao, ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa agizo la Serikali la kuepuka mikusanyiko ya watu isiyo lazima kutokana na janga la ugonjwa wa CORONA.

"Mkuu wa Wilaya yenu anawapenda sana , ameniagiza nije kuwaona na kuwaletea kile alichokiandaa , kwahiyo niseme kuwa Serikali yenu chini ya Uongozi wa Mhe. Rais Dkt John P. Magufuli inawapenda sana , kikubwa mjisikie huru kama walivyo watoto wengine, msirudi nyuma kwani kuondokewa na wazazi au kukosa malezi ya wazazi isiwe kigezo cha kuwarudisheni nyuma mnatakiwa msongo mbele ili nanyi myafikie malengo mliyojiwekea" Alisema Ruth.

Aidha alieleza kuwa wapo watu ambao wamekuwa wakitoa misaada kwa watoto au watu ambao wamekua wakizunguka mitaani na kuomba misaada, huo sio utaratibu mzuri na kusisitiza kuwa ni vyema mtu unapokuwa na tatizo na unahitaji msaada kufika katika ofisi za Serikali na kuonana na Maafisa Ustawi ili waweze kushauri njia bora za kuweza kusaidiwa.

Kwa upande wa Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Enedy Mwanakatwe, alisema ni vyema jamii ikawiwa kuchangia makundi ya watoto wenye mahitaji maalumu vikiwemo vituo vya watoto yatima kwani kundi hili linahitaji msaada wa kuwa karibu



*Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John, akiwa amembeba mtoto aliyetelekezwa na Wazazi wake mara baada ya kumfikisha katika Makao ya kulelea Watoto yatima na wenye mazingira magumu ya Mgolole katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika Juni 16, 2020.*

zaidi na jamii kutokana na wengi wao kupotelewa na wazazi au kutelekezwa na ndugu zao.

Mwanakatwe, alisema kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya ndugu wa watoto waliopo kwenye vituo na jamii kwa ujumla kutokuona umuhimu wa kuwatembelea na kuwajulia hali watoto licha ya elimu ambayo imekuwa ikitolewa mara kwa mara kwa kuona kuwa jukumu hilo ni la jamii kwa ujumla na sio Serikali peke yake au taasisi binafsi.

“Pindi inapotokea mtoto amefiwa na wazazi ndugu wamekuwa wakiwaleta watoto vituoni, wakishapokelewa ndio mwisho wa ndugu wa mtoto husika kufika kituoni kumjulia hali au pengine hata kusaidia mahitaji mbalimbali, jambo hili linasikitisha sana mtoto anakua pasipo hata kufahamu ndugu zake wakati hii ni haki ya mtoto kisheria.”Alisema Mwanakatwe.

Naye Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Sidina Mathias, alitoa rai kwa wamiliki wa vituo vya kulelea watoto kuhakikisha kuwa pindi wapatapo taarifa au wanapoletewa watoto waliotelekezwa au kupotelewa na wazazi ni vyema kufikisha taarifa kwa Maafisa ustawi kabla ya kuwapokea na kuanza kuwahudumia katika vituo vyao lengo ikiwa ni kuhakikisha kuwa Maafisa ustawi wanashirikishwa ili waweze kufuatilia kwa undani taarifa za watoto husika kwani kumekuwa na tabia ya wazazi kutelekeza watoto wakiamini kuwa watasaidiwa katika vituo vya kulelea watoto jambo ambalo sio sahihi.

Misaada iliyotolewa na Katibu Tawala ni pamoja na mchele kilo 200, mafuta ya kula lita 80 na Sukari Kilo 50 kwa makao ya watoto yote mawili.

# MKURUGENZI MANISPAA YA MOROGORO AWATAKA WATUMISHI KUWEKA MALENGO KATIKA UTENDAJI WA KAZI.

MKURUGENZI wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, amewataka Watumishi wa Manispaa ya Morogoro kuweka malengo katika Utendaji wa kazi ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi na kuiletea maendeleo Manispaa na Taifa kwa ujumla.

Hayo ameyasema wakati wa kuzindua mafunzo kwa Watumishi pamoja na Watendaji wa Kata kuhusu mfumo wa wazi wa mapito na tathmini ya Utendaji kazi wa Watumishi wa Umma (OPRAS) yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa.

Amesema kuwa mafunzo hayo yanaendeshwa kwa njia za majadiliano, maswali na majibu , pamoja na kubadilishana uzoefu .

Akizungumza mara baada ya ufunguzi wa mafunzo hayo , Lukuba, amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha washiriki kujadili maana, umuhimu na namna mfumo wa wazi wa mapito  na tathmini ya Utendaji kazi wa Watumishi



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro akifungua semina ya mafunzo ya OPRAS kwa Watumishi kwenye  Ukumbi wa Manispaa.*

wa Umma (OPRAS) kwa watumishi wa Umma unavyofanya kazi , kuwawezesha watumishi ambao ni wasimamizi wa kazi kubadilishana uzoefu kuhusu namna bora ya kuweka malengo ya utendaji kazi na kuwasimamia watumishi waliopo chini yao katika kuweka malengo ya utendaji kazi , kuwawezesha washiriki kwa vitendo katika kuweka makubaliano ya utendaji kazi , kufanya mapitio ya utendaji kazi ya nusu mwaka na upimaji wa utendaji kazi wa mwaka pamoja na kuongoza majadiliano ya watumishi kuhusu chan-

INAENDELEA UK... 14

# RC SANARE AONGOZA MAMIA YA WATU KATIKA KUMBUKUMBU YA WAHANGA AJALI YA MOTO MSAMVU.

INATOKA UK... 02

sehemu ya makaburi inatengenezwa vizuri na kuwa na mandhari ambayo wageni, ndugu na marafiki wakija kwa ajili ya kutembelea basi waone kuwa marehemu hawa wametendewa haki , kwahiyo Serikali kushirikiana na wadau imejitahidi katika hatua mbalimbali za kuhakikisha marehemu hawa wanathaminiwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa eneo hili kwa kuweka ukuta, mnara ambao una majina kwa ajili ya kumbukumbu pamoja na kujengea kaburi moja moja , niwaombe nyote mlioshiriki katika kumbukumbu hii kuendelea kushikamana pamoja kama Taifa katika kuwaenzi wale wote waliotangulia mbele za haki " Alisema RC Sanare. Aidha, aliwashukuru wananchi wote waliojitokeza kushiriki-

ana na Serikali katika hatua zote ambazo zilikuwa zinachukuliwa kuhakikisha marehemu hawa wanatendewa haki. Katika hatua nyingine , amewataka wale wote wanaohusika na ujenzi wa Makaburi hayo wahakikishe kazi hiyo inakamilika kwa ubora unaotakiwa na kwa wakati huku akiagiza kamati ya Maafa ya Wilaya kuendelea kusimamia na kuratibu mpango wa kuzuia majanga na kuchukua hatua za kukabiliana nayo pindi yanapotokea na kuhakikisha eneo hilo linaendelea kutunzwa na linakuwa salama wakati wote.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa, amesema siku ya Agosti 10, iliacha machungu makubwa na majeraha hivyo ameipongeza Serikali kwa kulifanya tukio hilo kuingia katika historia ya matukio makubwa ya majanga hapa



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare akisalimiana na mmoja wa wahanga wa ajali ya Moto aliyenusurika .*

nchini kwa ajili ya kuwakumbuka waliotangulia mbele za haki.

"Nipende kutoa salamu zangu kwa wananchi wa Wilaya ya Morogoro na takribani nchi nzima wanafuatilia tukio hilo la kihistoria kabisa katika Mkoa wetu, jambo hili Mkuu wa Mkoa lilitugusa sana, mimi wakati ajali inatokea nilikuwepo nikawa naripoti kwa nafasi nyingine kama mwandishi wa habari wa TBC,kilikuwa kipindi kigumu sana kwetu na ndugu waliopoteza wapendwa wao , sisi tulikuwa mstari wa mbele tukiona kila kilichoendela,watu 115 walipoteza maisha , kikubwa tuwe watulivu na kuwaombea dua ndugu zetu "Alisema DC Msulwa.

# DC MSULWA AWATAKA WATUMISHI KUFANYA KAZI KWA UADILIFU.



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa, akipokea taarifa za utekelezaji kwa Mkuu wa Wilaya Mstaafu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Regina Chonjo leo Juni 25,2020 wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya Ofisi yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Morogoro.*

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa , amewataka watumishi wa umma Wilaya ya Morogoro kufanya kazi kwa weledi na uadilifu na kuwaasa wasikimbie maeneo yao ya kazi badala yake wawe chachu ya mabadiliko na utatuzi wa changamoto wanazokutana nazo katika maeneo yao.

Hayo ameyazungumza Juni 25,2020 wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya Ofisi kati ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya

INAENDELEA UK... 11

# MANISPAA YA MOROGORO YATOA JUMLA YA MILIONI 517,800,000/= MIKOPO KWA VIKUNDI.

INATOKA UK... 03

awamu ya tano imekuwa pamoja sana na wananchi wanyonge hususani wajasiriamali na inawapenda sana na inathamini mchango mkubwa unaoletwa na wajasiriamali wadogowadogo katika kukuza pato la Taifa na ndio maana imeamua kutoa mkopo bila riba.

"Ni vyema mkajiuliza , ni wapi mtu unaweza kukopeshwa na kurejesha bila riba ?" Tuutendee haki mkopo huu na kurejesha kwa wakati ili kusaidia na wengine kupata fursa ya kukopo, tusimwangushe Rais wetu , yeye anatuonyesha kwa mfano : ni jasiri , mchapa kazi na anatekeleza kwa vitendo na kutoa matokeo makubwa bila woga, nasi hivyohivyo mkaitumie fursa hii ya mikopo mliyopewa kupata matokeo makubwa" Ameongeza DC Chonjo.




*Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Mstaafu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Regina Chonjo (katikati) akikabidhi hundi ya Shilingi Milioni 517,800,000/= kwa vikundi vilivyoomba mikopo Manispaa ya Morogoro. (kushoto) Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba, Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Enedy Mwanakatwe, Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John , aliyekuwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga pamoja na wanavikundi.*

Wakati akikabidhi Bajaji 2 kwa vikundi hivyo, DC Chonjo, alisema wapo baadhi ya Viongozi ni wabinafsi na wanatabia ya kuweka maslahi yao mbele huku akisema wakati Serikali inapotaka kuwanunulia vikundi vifaa wao wanatafuta namna ya kuwarubuni ili wanunue wao ambapo jambo hilo halikubaliki.

Alisema Serikali ya Mhe.Rais John Pombe Magufuli siyo ya kununua vitu feki,vifaa vyote

INAENDELEA UK... 16



*Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi Manispaa ya Morogoro , Steven Benedict , (aliyevaa shati jekundu) akiwa na wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi Manispaa ya Morogoro akipitia taarifa za Ujenzi wa Stendi Kuu ya Daladala Mafiga ikiwa ni ziara ya Kamati hiyo kukagua miradi ya Maendeleo.*



*Viongozi , Wakiongozwa na Afisa Elimu Msingi Manispaa ya Morogoro, Chausiku Masegenya ,wakiwa katika picha ya pamoja na Wananchi mara baada ya kumalizika kwa sintofahamu ya juu ya mmiliki aliyedaiwa kumiliki eneo la Msitu mdogo uliopo Kata ya Mzinga Mtaa wa Kidangawa maarufu kama Kongwa.*

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
HUDUMA KWA WATEJA
*SIMU NAMBA* **0734 039 300**

# HABARI PICHA KUONESHA MATUKIO MBALIMBALI



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, akipokea pesa kwa mjasiriamali ya malipo ya kitambulisho cha mjasiriamali mdogo*



*Watoto wakimuombea Dua Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, mara baada ya kupokea vyakula hivyo kwa ajili ya Sikukuu ya Eid Fitir.*



*Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood (kulia) akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa Kitabu cha Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2015/2020 katika kipindi chake cha muda wa miaka 5 ya Uongozi. (katikati) Mkuu wa Wilaya Mstaafu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Regina Chonjo. wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya Ofisi ya Mkuu wa Wialaya ya Morogoro.*



*Mmoja ya Wananchi wa Manispaa ya Morogoro akiweka saini katika zoezi la Uwekaji wazi Daftari la Awali la Wapiga kura linaloendelea leo Juni 18,2020 katika Kituo maalumu cha Kujiandikisha Wapiga kura Shule ya Msingi Mwere Manispaa ya Morogoro .*



*Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, (kulia), Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Enedy Mwanakatwe (kushoto ya mkurugenzi), Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Manispaa ya Morogoro, Bi Marry Kachale (wa pili kutoka kushoto) akiwa na viongozi wengine katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.*



*Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Loata Sanare (wapili kutoka kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa (kushoto), Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba (wapili kutoka kulia) wakiwa na Wakuu wa Idara Manispaa ya Morogoro katika ziara ya kukagua shule pamoja na maandalizi yaliyofanywa baada ya kufunguliwa kwa shule hizo.*



Mwakilishi wa Mkuu wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Jafari Makupula, akimkabidhi Cheti Bi, Yustina Wilbrod Mutafungwa (kulia) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wildina Foundation, wakati wa Kongamano la mfano la Wanawake lililoandaliwa na Ladiestalk Tanzania chini ya Mkurugenzi wa Taasisis hiyo Salome Sengo (katikati).



Mkurugenzi Manispaa Morogoro , Sheilla Lukuba, akipata maelezo ya kina juu ya kilimo cha Green House kutoka kwa Afisa Kilimo Manispaa ya Morogoro , Michael Waluse.

# DC MSULWA AWATAKA WATUMISHI KUFANYA KAZI KWA UADILIFU.

INATOKA UK... 08

ya Morogoro Mstaafu Mhe. Regina Chonjo na Mkuu wa Wilaya aliyepata uteuzi kwenye ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Morogoro.
Msulwa, amesema watumishi wa umma wana maarifa hivyo wanapaswa kutumia maarifa hayo kukabiliana na changamoto zinazowakabili badala ya kuhama maeneo ya kazi kwa kuwa Wananchi wanawahitaji kwa ajili ya kuwapa huduma wanazostahili.
Amesema ni vyema kila Halmashauri kujiwekea utaratibu wa kuwapongeza watumishi wanaotimiza wajibu wao vizuri ili kuongeza morali ya utendaji kazi kwa watumishi na kwa wale wanaokiuka maadili ya utumishi na kuwa wazembe katika kazi wapewe onyo kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa Umma.
"Utumishi wa umma ni fursa hivyo fanyeni kazi kwa weledi, uadilifu na ubunifu maana dunia inabadiilika na ndiyo maana tunasisitiza waajiri watoe mafunzo ya mara kwa mara ili watumishi waendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia,niwaombe mfanye kazi kwa uadilifu wa hali ya juu na kuacha kufanya kazi kwa maigizo" Alisema Mhe. Msulwa.
Aidha alisema Serikali inatarajia kuwa na watumishi wenye uadilifu uliotukuta katika jamii na utoaji huduma kwa wananchi, watumishi wanaowajibika kwa serikali nawananchi,



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ,Mhe. Bakari Msulwa, akipitia taarifa za Mwananchi anayedai kulimbikiziwa bili ya Maji , (kulia) Kaimu Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse.

nidhamu ya kazi kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, ndio dira ya serikali na itasimamia kuona kuwa utekelezaji unafanyika.

"Kila mmoja atimize wajibu wake, migogoro kwa kiasi kikubwa inazuirika kwani Serikali yetu ina mfumo mzuri kuanzia ngazi za chini hadi za juu, baadhi ya wataalamu wanakuwa vyanzo vya migogoro huku wananchi wakihangaika bila sababu , lakini pia wananchi hawapewi taarifa kwa wakati hili sio jambo jema, kiongozi mzuri ni yule aliye katika suluhu ya matatizo na sio sehemu ya matatizo, niwaombe wataalamu msisubiri viongozi wa kisiasa waje kutatua kero hizo fanyeni kazi na muwe makini katika kutatua migogoro kwa kutumia taaluma zenu ili wananchi muwape huduma bora na wafurahie matunda ya kuwa na Uongozi katika sehemu husika " Aliongeza Mhe. Msulwa.

Hata hivyo, alisema kuwa ni jukumu la kila mkuu wa Idara na kitengo kusimamia sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma ili kuweza kuleta maendeleo chanya kwa watu anaowasimamia na kuondoa kero na malalamiko yanayojitokeza mara kwa mara kwani kuna matatizo mengine ni madogo ambayo yako ndani ya uwezo wa mkuu wa idara au kitengo kuweza kuyatatua.

Alimalizia kwa kuwapongeza watumishi wa Halmashauri ya Morogoro kwa uwajibakaji na utendaji wao kazi uliotukuka na kuwataka kuendelea na moyo huo huo wa kuwatumikia wananchi wa Manispaa ya Morogoro ili kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi kulingana na sekta zao.

Kwa upande wa Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, amemshukuru Mkuu wa Wilaya kwa nasaha yake pamoja na maagizo kwa Watumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao ya kazi.




*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa (katikati) akifurahi na kuonyesha Jezi aliyozawadiwa na Mkurugenzi wa Fountain Gate Sports Academy baada ya uzinduzi wa Kituo hicho. (kushoto ) Mkurugenzi wa Fountain Gate Sports Academy , Japhet Makau (kulia ) Kaimu Afisa Michezo Manispaa ya Morogoro, Jimmy Katabaruki.*



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa (kulia) akitoa malekezo wakati wa kukagua mradi wa Soko Kuu la Kisasa Juni 25, 2020. (kushoto) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Mhe. Abdulaziz Abood, (katikati) Katibu wa Vijana UVCCM Egbona.*



*Wajumbe wa C.M.T Manispaa ya Morogoro wakiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro , Michael Waluse wakijadiliana mara baada ya kufika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Shule ya Msingi Kata ya Mzinga.*



*Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Bakari Msulwa, (aliyevaa suti nyeusi) akikata utepe kuzindua rasmi magari yaliyonunuliwa na Manispaa ya Morogoro pamoja na Magari ya usafishaji wa Mji kutoka Kampuni ya Kajenjere iliyopata dhabuni ya kufanya kazi hiyo, (kulia ) Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro Sheilla Lukuba., Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Enedy Mwanakatwe, Afisa Elimu Sekondari Manispaa ya Morogoro, Dr Janeth Barongo,aliyekuwa Afisa Utumishi Manispaa ya Morogoro Waziri Kombo.*

# MKURUGENZI MANISPAA YA MOROGORO ATAKA JAMII ISHIRIKI KATIKA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, ameitaka jamii ya Manispaa ya Morogoro kushiriki kwa vitendo katika ujenzi wa miundo mbinu ya elimu ili jamii iondokane na ujinga na kupata mafanikio ya haraka .

Kauli hiyo, ameitoa Julai 08,2020 , wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya Ujenzi wa Madarasa 2 pamoja na Jengo la Ofisi ya Waalimu katika Shule ya Sekondari SUA Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza na Waandishi wa habari, Lukuba, alisema ziara ya leo ni kukagua na kuangalia maendeleo ya Ujenzi wa Madarasa 2 na Jengo la Utawala ambapo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Loata Sanare, alitoa maagizo juu ya Ujenzi huo baada ya vuta ni kuvute baiana ya Kata mbili kufuatia kile kilichodaiwa ni mgogoro wa kimipaka

Lukuba, katika ziara hiyo amewasisitizia mafundi kwenda na kasi kubwa ili wanafunzi waanze kuyatumia madarasa hayo katika kupunguza msongamano darasani.

''ifike wakati sisi jamii ndio tuwe wa kwanza kuanzisha miradi kisha ndio serikali iwekeze nguvu zake, nimekuja kuona maagizo ya Mkuu wa Mkoa yanatekelezwaje, lakini na mwagiza Mhandisi wa Manispaa ya Morogoro aongeze kasi ya kuwasismamia mafundi, wanafunzi wetu wana uhaba wa madarasa hatutaki mrundikano, tunataka yakamilike wanfunzi wasome katika mazingira ya kuachiana nafasi na Waalimu wetu wakae katika Ofisi nzuri na rafiki ili kuongeza kasi ya ufaulu, ukiwa katika mazingira mabaya hata ile hali ya ufundishaji inashuka, kazi nimeiona inaendelea lakini ongezeni kasi tumalize kazi mapema" Amesema Lukuba.



*Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, akipiga Plasta ukuta wa Jengo la Ofisi ya Walimu Shule ya Sekondari SUA.*

Lukuba, amesema kuwa Jamii inaposhiriki ipasavyo kwa vitendo katika ujenzi wa miundo mbinu ya elimu huwa chachu ya kupata kilicho bora kabisa maana jamii huwa na uchungu nacho kutokana kuwekeza nguvu zao na huwa walinzi wakubwa.

''Nawagiza watendaji wa vijiji na kata kwa wale wote watakao taka kujitolea katika ujenzi huu wa taifa katika vijiji na kata ambapo miradi hiyo inafanyika fuateni sheria ndogo za vijiji zilizotungwa katika jamii zetu kwa weledi kabisa ili kufikia malengo ya mradi kwa jamii kushiriki sawa'' Ameongeza Lukuba.

Mwisho ametoa wito kwa wananchi wote wa Manispaa ya Morogoro kuwa tayari kujitolea kwa hiari katika miradi ya maendeleo.



Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba (katikati) wakishariana jambo na Afisa Elimu Sekondari Manispaa ya Morogoro, Dr Janeth Barongo (kulia) pamoja na Mkuu wa Shule ya Sekondari SUA , Mwl. Festo Kayombo wakati wa ukaguzi wa Ujenzi wa madarasa na Jengo la Utawala katika Shule ya Sekondari SUA.



Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii- TASAF, (National Steering Committee ) Eng. Rogatus Mativila, akikagua zoezi la uhakiki wa Kaya zilizo katika Mpango wa TASAF Manispaa ya Morogoro.

# MKURUGENZI MANISPAA YA MOROGORO AWATAKA WATUMISHI KUWEKA MALENGO KATIKA UTENDAJI WA KAZI.

INATOKA UK... 07

gamoto zao za kiutendaji kazi na mbinu za kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Amesema kuwa uanzishwaji wa OPRAS ni hatua muhimu kwa serikali katika kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma.

Aidha, amesema OPRAS ni chombo muhimu cha uwajibikaji kwa kila mtumishi ambacho kinasisitiza umuhimu wa USHIRIKISHWAJI, UMILIKI NA UWAZI ambapo watumishi wanahusisha katika kupanga malengo, utekelezaji, kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo na mchakato wa kufanya mapitio ya utendaji.

Lukuba amesema baada ya mafunzo hayo anatarajia kuwa watumishi wataweza kueleza maana , umuhimu na kanuni za usimamizi wa utendaji kazi (Performance Management ) katika utumishi wa Umma, kuonesha uelewa mpana juu ya mfumo wa wazi wa mapitio na tathmini ya utendaji kazi , kuonesha uelewa mpana wa kanuni za maadili katika utumishi wa Umma na kuzitekeleza kwa Vitendo katika maeneo yao ya kazi , kubuni njia bora za utoaji wa huduma kwa wananchi na watumishi wanaowasimamia kwa ufanisi na uadilifu pamoja na kuonesha uelewa na ubunifu katika utunzaji na matumizi ya kumbukumbu kwa ajili ya kufanya maamuzi mbalimbali.

Mbali na usimamizi wa utendaji kazi lakini matokeo ya mfumo huo ni mawasiliano ya mara kwa mara kati ya msimamizi wa kazi na mtumishi, na uelewa wa pamoja wa mahusiano yaliyopo kati ya malengo ya taasisi na yale ya mtumishi binafsi.

"Tumefungua rasmi mafunzo haya kwa watumishi wenu nafikiri kile ambacho kitafundishwa kitawasaidia sana katika utendaji wao wa kazi , lengo tunataka kuona matokeo chanya , mabadiliko haya ya kutathmini utendaji kazi wa watumishi wa umma yanakwenda sambamba na sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998 na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 ambazo zote zinasisitiza uwekaji wa mifumo ya menejimenti ya utendaji bora wa kazi inayojali matokeo ya kazi na kwamba maswala ya ajira, uteuzi na kupandishwa ngazi katika utumishi wa umma

yatakuwa kwa ushindani uwazi na unaozingatia sifa, ujuzi na uadilifu wa hali ya juu" Alisema Lukuba.
Mwisho, alisema mategemeo yake ni kwamba mwongozo huo wa OPRAS utatumika kama chombo cha watumishi katika taasisi za umma kujifunza jinsi ya kutumia na kutekeleza OPRAS kwa nia ya kuwa watendaji wanaojali zaidi matokeo bora katika utoaji wa huduma kwa umma.
Kwa upande wa Afisa Utumishi wa Manispaa ya Morogoro, Waziri Kombo, Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa OPRAS unaeleweka kwa pande zote za mwajiri na mwajiriwa, Manispaa ya Morogoro kupitia muongozo wa Serikali imefungua mafunzo haya kuhusu utekelezaji wa OPRAS katika Utumishi wa Umma.
Kombo alisema kuwa, mwongozo huu unatoa tafsiri ya maneno yatumikayo mara kwa mara na unatoa maelezo ya jinsi ya kujaza fomu ya OPRAS na jinsi ya kufanya mapitio na mwisho na kutumia matokeo ya mapitio na tathmini ya utendaji kwa mfano utoaji wa zawadi, adhabu na hatua za maendeleo kwa nia ya kuboresha utendaji wa mtumishi.
Katika hatua nyingine, Kombo, aliwataka Watendaji wa Kata kupitia katika maeneo ya biashara, maduka na vibanda pamoja na maeneo yenye mikusanyiko ya watu ili kuona kama watu wanafuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.
Naye mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Cliford Ringo, amewaomba watumishi kusikiliza kwa umakini kwa kuwa wao ndio viongozi wa ngazi za juu hivyo wasipo kuwa na uelewa mkubwa itakuwa vigumu kwenda kuwafundisha wengine huko waendapko na kupelekea mfumo huo kuonekana mgumu.
Akitoa mada katika mafunzo hayo, Dk. Ringo, alisema kuwa kumekuwa na changamoto mbalimbali katika matumizi ya OPRAS kwa watumishi wa Umma kitu kinachopunguza ufanisi katika kufikia malengo ya kazi.
Dk. Ringo, alieleza kuwa wameamua kutoa mafunzo hayo kutokana na changamoto zilizobainishwa ikiwepo kutokuwepo kwa uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa OPRAS kwa Watumishi wa Umma , kutokuwepo kwa usimamizi thabiti katika kuhakikisha mfumo huo unatekelezwa kama inavyotakiwa pamoja kutokuwepo kwa taratibu madhubuti katika kufanya ufuatiliaji na tathmini.
Mbali na changamoto alizozitaja amesema kuwa changamoto nyingine iliyobainishwa ni suala la ujazaji wa fomu ya OPRAS hususan katika kuweka usahihi wa malengo ya mtumishi unaoshabihiana na upimaji sahihi wa utendaji wa kazi.


Wanafunzi wa Shule za Msingi Azimio A na B Kata ya Kihonda Manispaa ya Morogoro , wakionesha furaha baada ya kukabidhiwa majaba ya maji na sabuni kwa ajili ya kujikinga na Ugonjwa wa CORONA.


Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Sidina Mathias, (kushoto), akikabidhi msaada kwa Mzee Sudi Ally aliyeunguliwa na Nyumba.

# MANISPAA YA MOROGORO YATOA JUMLA YA MILIONI 517,800,000/= MIKOPO KWA VIKUNDI.

INATOKA UK... 09

vipo kwenye viwango vinavyotakiwa , vyenye viwango bora ikiwa na lengo la kuhakikisha vinadumu kwa muda mrefu .

Pia aliwaagiza Maafisa Watendaji wa Kata na Maafisa Maendeleo ya Jamii wafuatilie na kusimamia mikopo iliyotolewa kwa vikundi kwani pesa hizo ni kodi za wananchi na ni lazima zirudishwe kwa wakati.

Mwisho aliendelea kuwasisitizia wananchi kuchukua hatua na kufuata taratibu zinazotolewa na wataalamu wa afya dhidi ya ugonjwa wa CORONA hususani watu wanapokuwa katika shughuli za uzalishaji.

Kwa upande wa aliyekuwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro na Diwani wa Kata ya Mazimbu, Mhe. Pascal Kihanga, alisema kuwa mikopo waliyopewa makundi hayo haina riba kwa hiyo wanapaswa kurejesha fedha kulingana na kiwango walichopata.

Kihanga, alisema kuwa lengo la mikopo inayotolewa ni kuwakomboa Vijana, Wanawake na Walemavu kutoka katika umaskini na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Nchi na kueleza kuwa kikundi kitakachorejesha mkopo kwa wakati kitapewa mkopo mwingine zaidi ya ule walioupata awali.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, alisema lengo la mfuko wa maendeleo ya Wanawake , Vijana na watu wenye Ulemavu ni kutoa fursa kwa jamii ili waweze kupata kwa urahisi mkopo usio na riba kwa wanavikundi kujidhamini wenyewe.

Lukuba alieleza kuwa mikopo hiyo hutolewa ili kuongezea kundi hilo kujiendeleza kiuchumi na kuinua hali za maisha ili kuendana na kauli mbiu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli ya kufikia uchumi wa kati.

“Kwa sasa Manispaa ya Morogoro imewapatia mikopo hii na nina imani kuwa mtaitumia mikopo hii vizuri kuboresha biashara zenu na kurejesha kwa wakati ili kuwezesha vikundi vingine viweze kukopa, kwa kufanya hivyo mtakuwa mmejenga imani na kufungua milango ya kuongezewa mikopo na hata kutoa fursa kwa wadau wengine wa maendeleo wanaojitokeza wenye nia ya kuwasaidia , wawasaidie kwa moyo” Alisema Lukuba.

Akitoa maelezo juu ya mikopo hiyo, Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Bi Enedy Mwanakatwe , alisema katika kipindi cha mwezi Juni Manispaa ya Morogoro imetoa mkopo wenye thamani ya Shilingi Milioni 245,800,000.00 ambapo kiasi cha Shilingi Milioni 110,900,000.00 kwa vikundi 44 vya Wanawake na Shilingi Milioni 103,500,000.00 kwa vikundi vya Vijana na Shilingi Milioni 31,400,000.00 kwa vikundi 6 vya watu wenye ulemavu.

Mwanakatwe alieleza kiasi cha Shilingi milioni 272,000,000.00 tayari zimetengwa kwenye akaunti ya Wanawake , Vijana na watu wenye Ulemavu ambapo mchakato wa vikundi vitakavyopatiwa mkopo huo upo katika hatua za mwisho.

“Vikundi vinavyopewa mikopo ni vile ambavyo vimependekezwa na kamati ya maendeleo ya kata na kufanyiwa uhakiki na kuonekana kuwa vinakidhi vigezo, lakini pia tumevipa vipaumbele vikundi vinavyofanya shughuli za viwanda vidogodogo ambapo katika mkopo huu tumewanunulia Bajaji (3) na Mizinga ya nyuki 114” Alisema Mwanakatwe.

Manispaa ya Morogoro imetoa Shilingi Milioni 517,800,000/= kwenye mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni mikopo ya vikundi mbalimbali vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu.



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**


OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 166
**MOROGORO TANZANIA**



(C) 2020

# AUTI YA MANISPAA MOROGORO












# JARIDA LA MWEZI

Mwezi Aprili - agosti 2020

Toleo namba 03